## DIRA, DHIMA NA MANUFAA

**Dira**


Taifa lenye Umwagiliaji endelevu unaochochea mapinduzi ya kilimo.

**Dhima**

Kubadilisha kilimo kupitia uratibu, udhibiti na uendelezaji wa Umwagiliaji endelevu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**Manufaa kwa Mkulima na Taifa**

- ✓ Uhakika wa maji na kilimo cha misimu yote.
- ✓ Ongezeko la uzalishaji na kipato cha kaya.
- ✓ Usalama wa chakula na malighafi za viwanda.
- ✓ Ajira na ukuaji wa uchumi vijijini.



**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

**S.L.P. 146, Njedengwa, Dodoma**

**Simu:**
+255 26 296 2073

**Barua Pepe:**
info@nirc.go.tz

**Facebook/Instagram/Twitter:**
Nirc_tz

**Youtube:**
Tume ya Taifa ya Umwagliaji

**Tovuti:**
www.nirc.go.tz



# TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI (NIRC)

## UJENZI NA UKARABATI MABWAWA YA UMWAGILIAJI

AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA | bbt Building a Better Tomorrow

## UTANGULIZI

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) inatekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya Umwagiliaji nchini kote ili kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha na ya uhakika kwa ajili ya kilimo cha Umwagiliaji.

Mabwawa haya huvuna na kuhifadhi maji ya mvua na mito ili yatumike wakati wa kiangazi, na hivyo kuwezesha kilimo cha misimu miwili au zaidi kwa mwaka.

### Kwa Nini Mabwawa?

- Kuvuna na kuhifadhi maji kwa matumizi ya Umwagiliaji wakati wote wa mwaka.
- Kuongeza uhakika wa uzalishaji wa mazao na kupunguza utegemezi wa mvua.
- Kuwezesha kilimo cha zaidi ya msimu mmoja na kuongeza tija kwa mkulima.
- Kudhibiti mafuriko na kulinda miundombinu ya chini ya bonde.



## HATUA ZA MRADI WA BWAWA

Kila mradi wa bwawa hupitia hatua zifuatazo kabla na wakati wa ujenzi:

**1. Upembuzi Yakinifu na Usanifu.**

Wataalam hufanya tathmini ya eneo, upatikanaji wa maji, na kubuni usanifu wa bwawa.

**2. Mchakato wa kumtafuta Mzabuni/Mkandarasi.**

Mchakato wa kumpata mkandarasi na mshauri elekezi wa ujenzi.

**3. Ujenzi na Ukarabati.**

Ujenzi wa tuta la bwawa, spillway, na miundombinu ya kuchukua na kusambaza maji.

**4. Ukamilishaji na Ukabidhi**

Bwawa hukamilishwa, kufanyiwa ukaguzi, na kukabidhiwa kwa umoja wa wamwagiliaji.

### TAKWIMU KWA MUHTASARI (HALI YA MABWAWA)

| KIPENGELE | IDADI | MAELEZO |
|---|---|---|
| Mabwawa kwenye ujenzi/ukarabati | 22 | Wakandarasi wanaendelea |
| Mabwawa katika usanifu/manunuzi | 92 | Mbioni kuanza utekelezaji |
| Mikoa inayonufaika | 25 | Tanzania Bara |
| Mabwawa yaliyokamilika | 2+ | Tlawi, Ulyanyama, Nyida |



### MIFANO YA MABWAWA YANAYOJENGWA

Baadhi ya Mabwawa Yanayojengwa/Kukarabatiwa

| BWAWA / MKOA | WILAYA | MAENDELEO |
|---|---|---|
| Tlawi / Manyara | Mbulu | 100% - Ujenzi umekamilika |
| Ulyanyama / Tabora | Sikonge | 100% - Ukarabati umekamilika |
| Msagali / Dodoma | Mpwapwa | 98% – Ujenzi unaendelea |
| Membe / Dodoma | Chamwino | 98% – Ujenzi unaendelea |
| Kasoli,Simiyu | Bariadi | 92% – Ujenzi unaendelea |
| Katunguru / Mwanza | Sengerema | 98% - Ujenzi umekamilika |
| Nyida / Shinyanga | Shinyanga | 98% - Ujenzi umekamilika |
| Mkomazi / Tanga | Korogwe | 98% - Ujenzi unaendelea |

Mabwawa mengine yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika mikoa ya Lindi, Kigoma, Geita, Simiyu, Singida, Arusha na Mtwara.

